**JAMHURI YA KENYA** **SERIKALI YA KAUNTI YA NAROK**

**OFISI YA MWANASHERIA WA KAUNTI**

***S.L.P 898-20500-NAROK-*** *NAMBARI YA SIMU.****0721788-818*** *BARUA PEPE:*
**legal@narok.go.ke** TOVUTI*: www.narok.go.ke*

---

## HATI YA UTOAJI WA HUDUMA KWA WANANCHI KATIKA OFISI YA MWANASHERIA WA KAUNTI

### Dira Yetu

Kituo bora cha ubora katika kuhimiza na kulinda utawala wa sheria na utawala bora.

### Dhamira Yetu

Kutoa huduma za kisheria kwa wakati, kwa uwazi na ufanisi ili kuhimiza utawala bora na kuheshimu utawala wa sheria**.**

### Malengo Yetu Ya Kistratejia

**Malengo yetu ya kitratejia ya idara ni:**

i. Kutoa huduma bora za kisheria kwa serikali na umma;

ii. Kuhimiza utekelezaji wenye ufanisi wa katiba;

iii. Kuchunguza na kubuni/kuandaa upya mikakati ya ndani ili kuendana na mahitaji yanayobadilika ya kisheria naya udhibiti;

iv. Kutoa ushauri wa kisheria kuhusu uandaaji wa sheria na masuala mengine ya kisheria; na

v. Tunahimiza uhifadhi wa viwango vya maadili katika kaunti yetu.

| No | HUDUMA ZINAZOTOLEWA | VIGESO VYA KUPATA HUDUMA | GHARAMA | MUDA WA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kupokea mgeni kwa ofisi ya mwanasheria. | Maelezo ya wageni | Hakuna | Dakika mbili |
| 2 | Kutoa huduma kwa mgeni | Maoni kutoka kwa wageni | Hakuna | Dakika kumi na tano |
| 3 | Kumwelekeza mgeni katika ofisi husika | Uthibitisho kutoka kwa ofisi inayohusika | Hakuna | Dakika tano |
| 4 | Upokeaji na uelekezaji wa malalamiko na wapaji wa maombi | Taarifa za wapaji wa maombi/walalamikaji na asili ya malalimiko | Hakuna | Dakika ishirini |
| 5 | Uratibu na uwezeshaji wa huduma za mapokezi kwa ajili ya shughuli rasmi za idara | Maombi rasmi kutoka kwa idara | Hakuna | Dakika kumi |
| | **UTAWALA WA JUMLA** | | | |
| **No** | **HUDUMA ZINAZOTOLEWA** | **VIGEZO VYA KUPATA HUDUMA** | **GHARAMA** | **MUDA WA UTEKELEZAJI** |
| 1 | Uwasilishaji rasmi wa sera za serikali kwa idara husika | Hakuna | Hakuna | Siku moja |
| 2 | Ushughulikiaji wa malalamiko na maombi ya umma | Malalamiko na maombi rasmi kutoka kwa wateja | Hakuna | Siku tano |
| 3 | Uthibitisho rasmi wa kupokea mawasiliano | Mawasiliano rasmi kutoka kwa wateja | Hakuna | Siku moja |
| 4 | Majibu kwa mawasiliano rasmi | Mawasiliano rasmi kutoka kwa wateja | Hakuna | Siku moja |
| 5 | Urejeshaji rasmi kwa kumbu kumbu na nyaraka | Maelezo rasmi ya kumbukumbu na nyaraka | Hakuna | Dakika ishirini |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| **MAJUKUMU YA KIMSINGI** | | | | |
| **No** | **HUDUMA ZINAZOTOLEWA** | **VIGEZO VYA KUPATA HUDUMA** | **GHARAMA** | **MUDA WA UTEKELEZAJI** |
| 1 | Uwakilishi wa utawala wa kaunti mahakamani | a) Utoaji wa maelekezo yenye uwazi na ufafanuzi kamili<br>b) Nakala za nyaraka na mawasiliano muhimu yanayohusiana | Hakuna | Kulingana na kanuni za utaratibu zinazotawala na maagizo ya mahakama |
| 2 | Uweseshaji wa mfumo wa utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala (ADR) | a) Utoaji wa maelekezo yenye uwazi na ufafanuzi kamili<br>b) Nakala za nyaraka na mawasiliano muhimu yanayohusiana | Hakuna gharama inayotozwa na idara<br>Mengineyo ya gharama kama yatakavyoelekezwa na mahakama ya usuluhishi | Kulingana na maagizo ya mahakama ya usuluhishi |
| 3 | Kuandaa na uhakiki wa sheria,ikiwemo,sera,miswaada na kanuni mengineyo | a) Kupokelewa kwa maelekezo ya rasimu ya sheria kutoka kwa idara za kaunti<br>b) Kupokelewa kwa nyaraka husika | Hakuna | Katika kipindi cha siku arobaini na tano |
| 4 | Majadiliano,uandaaji na uhakiki wa makubaliano ya kisheria (mikataba, makubaliano ya m.o.u, na vyombo vingine | a) Kupokelewa kwa maelekezo ya rasimu ya sheria | Hakuna | Mchakato endelevu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kutoka kwa idara za kaunti<br><br>b) Kupokelewa kwa nyaraka husika | | |
| 5 | Huduma rasmi za ushauri wa kisheria | Kwa maombi rasmi na kulingana na uhitaji | Hakuna | Mchakato endelevu |